



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS,  
TAWALA LA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA SIHA



Unapojibu tafadhali taja:  
Kumb.Na. SDC/C.50/5/19

21 Februari, 2022

**TANGAZO NAFASI YA KAZI AJIRA YA MUDA UKUSANYAJI TAARIFA  
ANWANI ZA MAKAZI (POSTIKODI)**

Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Siha anawatangazia nafasi za **ajira ya muda** kwa nafasi za kukusanya Taarifa kwenye zoezi la Mfumo wa Anwani za Makazi katika Kata, Vijiji na Vitongoji vyote ya Halmashauri ya Wilaya ya Siha.

**1. SIFA ZA WAOMBAJI**

- i. Awe Raia wa Tanzania mwenye Umri kati ya Miaka 18-45
- ii. Awe na Elimu kuanzia kidato cha Nne na kuendelea
- iii. Awe anamiliki Simu Janja (Smartphone) android yenye uwezo wa kukaa na chaji kwa siku nzima pamoja na uwezo wa kupokea mfumo wa anwani za Makazi. Aidha, mwenye kishkwambi (tablet) atapewa kipaumbele Zaidi.
- iv. Awe na Barua pepe(email address) na Nywila (password) inayofanya kazi.
- v. Awe na uwezo wa kusoma ramani za Mitaa.
- vi. Awe ni Mkazi wa Kata/Kijiji/Kitongoji husika.

**2. MAJUKUMU YA KAZI**

- i. Kugawa na kuandika Namba za nyumba, Viwanja na Maeneo ya huduma
- ii. Kukusanya Taarifa za nyumba, Viwanja na Maeneo ya huduma
- iii. Kukusanya taarifa za Wamiliki wa Nyumba, Viwanja na Maeneo ya huduma kwa kutumia mfumo wa Anwani za Makazi
- iv. Kutuma Data kwenye mfumo wa Anwani za Makazi wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha.

**3. MAOMBI YAAMBATANISHWE NA;**

- a) Nakala ya cheti cha Kidato cha Nne na kuendelea
- b) Nakala ya Cheti cha kuzaliwa
- c) Picha mbili za pasipoti (passport size 2)

#### 4. JINSI YA KUTUMA MAOMBI

Barua zote za maombi ziandikwe kwa mkono zikiwa na Anwani kamili ya Mwombaji, Namba ya simu na barua pepe. Pia barua zote zipitie kwa Watendaji wa Vijiji na Kata anapoishi mwombaji na Barua ziwasilishwe Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Siha kwa anwani ifuatayo;-

**MKURUGENZI MTENDAJI,  
HALMASHAURI YA WILAYA YA SIHA,  
S.L.P 129,  
SANYA JUU - SIHA  
KILIMANAJARO.**

#### 5. TAREHE YA MWISHO KUPOKEA MAOMBI

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **28/02/2022 saa 9:30 alasiri.**

NB. Tangazo hili pia linapatikana katika Tovuti ya Halmashauri [www.sihadc.go.tz](http://www.sihadc.go.tz)



Mangali U.E

**MKURUGENZI MTENDAJI  
HALMASHAURI YA WILAYA YA SIHA**

DISTRICT EXECUTIVE  
DIRECTOR  
SIHA